TANGAZO LA SERIKALI NA. 23 la tarehe 17/02/2017

SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu Na. 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) HALMASHAURI YA WILAYA YA MALINYI MWAKA 2017

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi za Mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo-

“*Afisa Mwidhiniwa*” maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

“*Halmashauri*” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi;

“*Kibali*” maana yake ni idhini au ruhusa inayotolewa

na Halmashauri kuruhusu uchimbaji wa Madini ya Ujenzi;

"*Madini ya Ujenzi*" maana yake ni Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi.

"*Maeneo marufuku*" ni maeneo ya mito, madaraja, barabara, mashamba ya watu, mijini, maeneo ya shule, na maeneo mengine yanayofanana na hayo;

"*Mkurugenzi*" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

## SEHEMU YA PILI

## JINSI YA KUTOZA USHURU

Ushuru wa Madini ya Ujenzi,

4. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa madini ya ujenzi kutoka kwa wachimbaji wa madini, wauzaji au wasafirishaji waliopo katika eneo la mamlaka ya Halmashauri kwa viwango na taratibu zilizowekwa na Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru wa madini ya ujenzi utatozwa katika eneo la machimbo au eneo lolote ndani ya Mamlaka ya Halmashauri pale yatakapokutwa kuwa hajalipiwa ushuru.

(3) Wakati wowote itakapoona inafaa Halmashauri itakuwa na uwezo wa kubadilisha kwa kuongeza au kupunguza viwango vya Ushuru wa madini ya ujenzi kwa kuzingatia taratibu za kisheria.

Kibali na masharti ya kuchimba madini ya ujenzi

5. (1) Halmashauri itatoa kibali baada ya kupokea maombi ya kuchimba au kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri;

(2) Kibali kitakachotolewa kitaeleza aina ya madini ya ujenzi yatakayochimbwa na eneo yatakayochimbwa;

Maeneo ya Madini ya Ujenzi.

6. (1) Halmashauri itatenga na kutangaza maeneo yanayoruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi;

(2) Halmashauri inaweza kusimamisha shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi endapo itathibitika kwamba uchimbaji huo unaweza kuhatarisha usafi na uhifadhi ya mazingira au usalama wa wakaazi wengine wa eneo hilo

Maeneo yaliyopigwa marufuku

7. Ni marufuku kwa Mtu yeyote kuchimba madini ya ujenzi katika maeneo yafuatayo-

(a) Maeneo ya hifadhi;

(b) Maeneo ya mito au kando ya mito na vyanzo vya maji;

(c) Maeneo ya karibu na makazi ya watu;

(d) Maeneo ya hifadhi ya Barabara; na

(e) Maeneo ambayo yametajwa katika Sheria yoyote andishi kuwa haifai kwa shughuli ya uchimbaji wa madini ya ujenzi.

Muda na mahali pa kulipia ushuru

8. (1) Ushuru wa madini ya ujenzi utalipwa wakati gari linapotoka katika eneo yanapochimbwa madini hayo au sehemu yeyote litakaposimamishwa na Afisa Mwidhiniwa.

(2) Muda wa kukusanya Ushuru wa madini ya ujenzi ni kuanzia saa 12 kamili asubuhi mpaka saa 1 kamili usiku.

Uteuzi wa Wakala

9. (1) Halmashauri inaweza kumteua Mtu binafsi, Kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ushuru wa madini ya ujenzi kwa niaba yake;

(2) Wakala aliyeteuliwa atakuwa na majukumu ya-

(a) Kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmshauri katika eneo alilopangiwa, na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(b) Kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa mujibu wa Mkataba wa Uwakala alioingia na Halmashauri.

(c) Kumchulia hatua za kisheria Mtu, Kampuni, Shirika au Taasisi yeyote itakayokiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi.

## SEHEMU YA TATU
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa

10. Mtu yeyote ikiwa ni mnunuzi au muuzaji ambaye-

(a) atakataa au kukwepa kulipa ushuru;

(b) atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu wasilipe ushuru

(c) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake;

(d) atachimba Madini ya ujenzi mahali ambapo hapajaruhusiwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(e) atadanganya na kuhusiana na kitendo chake hicho ataikosesha Halmashauri mapato yake;

Adhabu

11. Mtu yeyote ambaye atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu Hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

12. (1) Mkurugenzi wa Halmashauri anaweza kufifilisha kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, iwapo Mkosaji kwa hiari yake mwenyewe atakiri kwa maandishi na kukubali kulipa faini isiyozidi Shilingi Elfu Hamsini pamoja na kutekeleza wajibu aliouvunja.

(2) Halmashauri inaweza kuruhusu Madini ya ujenzi kuchimbwa au kusombwa bila kulipwa ushuru kwa kibali maalum kitakachotolewa na Mkurugenzi.

Hati ya kukamata na kuuza kwa mnada mali ya mdaiwa

13. Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuomba katika Mahakama yenye Mamlaka katika eneo la Halmashauri kukamata na kuuza mali ya mdaiwa inayohamishika baada ya kupata kibali cha mahakama kwa kutumia fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

______

JEDWALI LA KWANZA

______

*(chini ya kifungu cha 4(1)*

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| *Na* | *Uzito wa gari* | *Uzito* | *Kiasi cha Ushuru* |
|---|---|---|---|
| 1. | Changarawe | tani 3 hadi 7 | 5,000/= kwa kila safari |
| 2. | Kokoto | tani 3 hadi 7 | 5,000/= kwa kila safari |
| 3. | Mchanga | tani 3 hadi 7 | 3,000/= kwa kila safari |
| 4. | Kifusi/ udongo wa kutengenezea tofali | tani 3 hadi 7 | 3,000/= kwa kila safari |
| 5. | Udongo wa saruji | tani 3 hadi 7 | 3,000/=kwa kila safari |

______

JEDWALI LA PILI

______

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 12)*

Mimi …………………… nakiri **KWA HIARI YANGU MWENYEWE** mbele ya ………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Malinyi, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi za Mwaka 2016.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurgenzi Mtendaji wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

**NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU**

Leo tarehe…………. ya Mwezi………… Mwaka ………………….
*Jina.………………………………..*
*Saini.…………………………………….*
Mbele ya :
Jina: ……………………………… Cheo: ………………………
Saini: ……………………………..

---

JEDWALI LA TATU

---

HALMASHAURI YA WILAYA YA MALINYI

HATI YA KUKAMATA MALI NA KUIUZA

***(**limetengenezwa chini ya Kifungu cha 13)*

JINA LA MALI: ……………………………………………………………………….

**KWA DALALI WA MAHAKAMA**

**…………………………………………………………………………………………..**
**…………………………………………………………………………………………..**

Hii ni kukuamuru kukamata na kuitunza mali inayoondosheka ya ……………………………….……………… ……………………………………………………………………………… ambayo imeonyeshwa katika Jedwali, mpaka mtajwa hapo juu atakapolipa shilingi……………………………………………………………………………….. zikiwa ni deni la kodi analodaiwa pamoja na riba kwa kiwango cha asilimia moja [1%] kwa kila mwezi kuanzia tarehe……………………… mwezi……………………………….. Mwaka. ……………………….. Mpaka tarehe…………………………..mwezi……………………… mwaka……………………………………… ikiwa ni pamoja na gharama za kukamata mali hiyo. Na baada ya kutoa taarifa [notice] ya siku kumi na nne ambayo itabandikwa katika jengo la mahakama na baada ya kumalizika kwa notisi hiyo, mauzo ya mali hiyo yataanza kwa mnada ili kupata shilingi…….……………………………………….pamoja na riba na gharama za kukamatia mali hiyo.

UNAAMRIWA kurudisha hati hii mnamo au kabla ya tarehe……………… mwezi………………………….. mwaka………………………………………. Pamoja na maelezo ya namna ulivyotekeleza amri hiyo au sababu kwanini hukutekeleza.

Imetolewa na mimi na kugongwa mhuri wa Mahakama leo tarehe……………………… Mwezi……………………………………… Mwaka…………………………………
……………………………………………………………………………………….

**HAKIMU**

Nembo ya halmashauri ya Wilaya ya Malinyi imebandikwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia azimio la Halmashauri iliyotolewa katika kikao kilichofanyika tarehe 23.04.2016 na ilibandikwa mbele ya:-

SAID ALLY MSOMOKA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi.*

FADHILI NASSORO LIGUGUDA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi.*

NAKUBALI,

Dodoma,
09Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
*Waziri wanchi-or-Tamisemi.*